

Maswali

1. Wanafunzi walikuwa wakiambia kila mtu nini?
2. Mfalme muovu alikuwa nani?
3. Herode alifanyaje Petro?
4. Herodi alikuwa anaenda kufanya nini siku ifwatayo?
5. Nani alikuja kuona Petro gerezani?
6. Petro alitokaje gerezani?
7. Petro alipokuwa huru alienda wapi?
8. Marafiki wa Petro walikuwa wanafanya nini?
9. Nani alikuja mlangoni?
10. Mbona Roda hakufungulia Petro mlango?
11. Mungu alikuwa amejibu maombi yao namna gani?

Majibu

1. Juu ya vile
2. Yesu alikuwa amefufuliwa kutoka kwa wafu na Ufalme wa Mungu.
3. Herode ndiye alikuwa mfalme muovu.
4. Herode aliweka Petro gerezani.
5. Herode alikuwa anaenda kuua Petro.
6. Malaika alikuja kuona Petro gerezani.
7. Minyororo zilianguka kutoka kwa mikono yake. Malaika alimchukua na wakapita vikundi viwili vywa walinzi bila kuonekana. Lango la chuma lilifunguliwa lenyewe.
8. Petro alienda kwa nyumba ya rafiki yake.
9. Walikuwa wanaomba ili Mungu aokoe Petro kutoka kwa gereza.
10. Roda alikuja kwa mlango.
11. Roda alifurahi sana. Alikimbia kwenda kuambia marafiki kwamba Petro ako kwa mlango.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 3



48 Petro gerezani

Marejeo

Matendo ya Mitume 12: 1 – 19

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu anaweza kulinda watu wake anaowapenda hata kama yanaonekana hayawezekani kwetu sisi.

Maneno maalum

- 48.1 Wanafunzi + ambia kila mtu + Yesu yu hai + Ufalme + Herode muovu + Wakristo + gereza
- 48.2 Herode + Petro + gereza + marafiki + ombo
- 48.3 Petro + walinzi wawili +malaika + minyororo ilianguka + kuja + fungua lango + Petro ako huru
- 48.4 Petro + nyumba ya rafiki + Roda + ombo + hawakuamini + endelea kugonga + kubali Petro aingie + Mungu alijibu maombi +Petro ako huru + shukuru Mungu

48.1 Yesu aliambia wanafunzi wake waambie kila mtu juu ya kifo chake, ufuluo wake na Ufalme wa Mungu. Kulikuwa na mfalme muovu sana aliyetawala Israeli, jina lake alikuwa Herode.

Wanafunzi walikuwa wakiambia kila mtu kwamba Mungu alimfufua Yesu kutoka kwa wafu. Waliwambia watu juu ya Ufalme waajabu wenye Yesu atakuja kusimamisha hapa duniani atakaporudi. Popote wanafunzi walienda waliambia watu juu ya Yesu. Hatimaye karibu kila mtu Yerusalemu katika nchi ya Israeli alikuwa amesikia ni nini wanafunzi walihubiri juu ya Yesu. Mfalme Herode naye pia alisikia juu yake. Herode muovu aliwakamata Wakristo waumini na wanafunzi na kuwaweka gerezani.

48.2 Herode alikamata Petro na akamweka gerezani. Petro alipokuwa gerezani alichungwa sana. Herode alipanga kuua Petro. Lakini marafiki wa Petro na wanafunzi wenzake walikuwa wakimwombea na Mungu alikuwa akimlinda.

48.3 Usiku kabla Herode amuuwe, Petro alikuwa amelala gerezani. Alikuwa amefungwa kwa walinzi wawili, mmoja kila upande wake. Punde tu aliamka na kuona mwangaza mwingi umemzunguka. Alikuwa malaika. Mungu alisikia maombi ya marafiki wa Petro. Kwa hivyo Mungu alikuwa ametuma malaika mmoja ili aje amwokoe. Malaika aliambia Petro, “Haraka, amka!” Halafu minyororo ilianguka kutoka kwa mikono ya Petro.

Malaika aliendelea kumwambia, “Vaa viatu vyako na joho lako, na unifuate.” Petro hakuamini macho yake alipoona minyororo ikianguka kutoka kwa mikono yake. Alifikiria kwamba ni lazima awe anaota. Lakini akafanye chenye malaika alikuwa anamwambia.

Walipita katikati ya vikundi viwili nya walinzi na hawakuwaona. Walipofika kwa lango kubwa la gereza na ni la chuma, lilifunguka lenyewe. Walitembea wakapita kwa hilo lango la chuma kimya mpaka kwa njia ya mji. Hakuna aliyejaribu kuwasimamisha. Petro alikuwa huru!

48.4 Baada ya kutembea kwa hatua kidogo malaika alimuacha. Petro alienda taratibu mpaka kwa rafiki yake. Aligonga kwa mlango, na msichana aitwaye Roda alikuja kuona aliyejukwa akgonga.

Marafiki wote wa Petro walikuwa kwa nyumba. Wote walikuwa wakiomba ili Petro aachiliwe. Lakini Yule msichana aliposikia sauti ya Petro, alifurahi, badala ya kufungua mlango, alirudi nyuma. Roda alikimbia na kwenda kuambia marafiki wake kwamba Petro alikuwa mlangoni.

Ingawaje walikuwa wakiombea Petro, hawakuamini. Lakini Petro aliendelea kubisha mlango. Waliposikia sauti ya Petro, wote walikimbia na kumfungulia mlango. Walijua kwamba Mungu alikuwa amesikia maombi yao na ameyajibu. Walifurahi sana kuona kwamba Mungu amemwokoa Petro. Walishukuru Mungu sana kwa kumwajilia Petro kuwa huru.

